

1) Wote tumetenda dhambi

WARUMI 3:23 kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;

2) Malipo yetu kwaajili ya dhambi zetu ni kifo

WARUMI 6:23 Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.

3) Sisi wote tunastahili kwenda jehanamu kulingana na Biblia

UFUNUO WA YOHANA 21:8 Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na waujaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili.

4) Kuna matumaini kupitia damu ya Yesu Kristo

WARUMI 5:8 Bali Mungu aonyesha pendo lake ye ye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenyewe dhambi.

5) Weka imani yako katika Yesu Kristo.

MATENDO YA MITUME 16:30-31 kisha akawaleta nje akasema, Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka? Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako.

YOHANA 3:18 Amwaminiye ye ye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.

YOHANA 3:16 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

I WATHESALONIKE 1:9 Kwa kuwa wao wenyewe wanatangaza habari zetu, jinsi kulivyokuwa kuingia kwetu kwenu; na jinsi mlivymgeukia Mungu mkaziacha sanamu, ili kumtumikia Mungu aliye hai, wa kweli;

6) Ni zawadi ya milele kutoka kwa Mungu.

WAEFESO 2:8-9 Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.

7) Sasa unajua jinsi ya kwenda mbinguni

I YOHANA 5:13 Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu.

Muombe Mungu akuokoe kupitia jina la Jesu **WARUMI 10:10 Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.**